

## **UDHIHIRIKAJI WA MAMLAKA NA MAHUSIANO YALIYO NA UBISHI KUPITIA DHAMIRA NA NAMNA KATIKA USEMI**

**Teresia W. Waweru, John Habwe & Iribe Mwangi**

### **Ikisiri**

*Makala inahusu dhamira na namna katika usemi na udhihirikaji wa mamlaka na mahusiano yanayoweza kutokana na matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kanisa Katoliki kwenye nyumba za watawa za malezi. Kanisa Katoliki ni mojawapo ya asasi zenye desturi, sheria, itikadi, imani na kanuni zinazoliongoza. Uongozi wake hutekelezwa kutegemea ngazi zilizoko. Mojawapo ya viungo muhimu vya kanisa ni jamii ya watawa wenye viongozi katika mashirika kama Mama Mkuu, Makamu wa Mama Mkuu, Wasaidizi wa Mama Mkuu (washauri), viongozi wa maeneo na walezi. Aidha, kuna watawa walioweka nadhiri za daima, nadhiri za muda na walelewa. Watawa hutumia lugha ya Kiswahili katika mitagusano inayozalisha mahusiano kati yao. Kila lugha hudhihirisha itikadi na mamlaka na hutegemea nafasi ya mshirika katika asasi fulani kama nafasi ya kiongozi, daktari na washirika kudhihirisha lugha ya mamlaka waliyonayo (Fairclough, 1992). Ngazi za kiutawala kwa watawa zinadhahirisha mamlaka yaliyopo ya kitawa kupitia matumizi ya lugha ya Kiswahili katika usemi. Kutokana na hoja hii kulidhihirika ubishi katika mahusiano ya kimamlaka wakati wa mawasiliano baina ya walezi na walelewa katika usemi kupitia matumizi ya lugha ya Kiswahili (Wodak, 2001). Data zilikusanywa nyanjani katika nyumba za kitawa katika Jimbo Kuu la Mombasa katika Shirika la Masista wa Mt. Yosefu ambapo lugha ya Kiswahili hutumika kwa mapana. Matini hizi ziliangaliwa katika kiwango cha kishazi na sentensi kupitia dhamira na namna kwa mtazamo wa Sarufi Amilifu Msonge. Nadharia hii inajihusisha na wazo la uamilifu wa lugha. Je, kuna uwezekano wa ubishi wakati wa mawasiliano kati ya walezi na walelewa kwenye nyumba za watawa za malezi? Je, mamlaka na mahusiano hudhihirika vipi katika matumizi ya lugha yaliyo rasmi na yasiyo rasmi katika nyumba za watawa za malezi? Maswali haya ndiyo yalijibiwa katika makala.*

### **Utangulizi**

Lugha ni kiungo muhimu kinachotumiwa katika nyanja na miktadha mbalimbali ya kijamii. Mzungumzaji huitumia lugha kwa nia ya kufanikisha mawasiliano pamoja na utangamano wa kijamii hasa katika usemi na mahusiano ya kimamlaka. Usemi ni muhimu katika kuelewa muktadha wa kinachozungumziwa na kuelewa pamoja na kukuza uhusiano kati ya msikilizaji na mzungumzaji. Muktadha wa kinachozungumziwa unaweza kutumia lugha kusababisha mabadiliko kupitia udhihirikaji wa ubishi. Ubishi na mahusiano ya jamii vinaweza kudhihirika

kupitia dhamira na namna. Dhamira na namna ni vipengele muhimu vya kujadili ili kuvielewa katika matumizi ya lugha na ukuzaji wa mahusiano ya kijamii.

Kwa mujibu wa Fairclough (1989, 2010), dhamira na namna ni muhimu kwa kuwa swali kuhusu kile watu wanachojihusisha nacho wakati wanatoa kauli, kuuliza maswali, kutoa amri, kushauri au hata kutoa maelekezo ni muhimu katika uundaji na uhifadhi wa mahusiano kati ya mzungumzaji na msikilizaji kama ilivyo kati ya mlezi na mlelewa. Dhamira huchangia katika nafasi ambayo mwandishi au mzungumzaji huchagua katika tukio la usemaji na majukumu anayompa msikilizaji. Kwa mfano, ikiwa mzungumzaji ataamua kutumia dhamira ulizi anachukua jukumu la yule anayeuliza maswali na anamweka msikilizaji katika nafasi ya yule anayetakiwa kujibu maswali, hivyo kumfanya mzungumzaji kuonekana kama aliye na mamlaka. Dhamira, kwa hivyo, siyo muhimu tu kwa kutafuta ni mawazo gani yanatiliwa mkazo au yasiyotiliwa mkazo katika usemi fulani lakini katika kudhihirisha jinsi watu wanavyojitambulisha na kujipatia nafasi katika usemi husika.

Kwa upande mwingine, namna inahusiana na uamuzi kati ya ‘ndiyo’ na ‘la’ ambayo inaeleza aidha hukumu ya mzungumzaji isiyo na upendeleo kuhusu kinachozungumzwa au katika kuonesha mahusiano ya kijamii, mahusiano ya kimamlaka na viwango vya urasmi. Namna, aidha, ni muhimu kwa kuangalia mahusiano ya kimamlaka kwa kuwa kupitia namna kuna uwezekano wa kujua, kwa mfano, ni dhana zipi zinakaziwa au kutokaziwa kuhusu mamlaka. Namna ni mtazamo wa mzungumzaji au mwandishi kuhusu ulimwengu. Mzungumzaji au mwandishi anaweza kudhihirisha uhakika, utayari, uwezekano, wajibu, lazima na uwezo kwa kutumia maneno ya hali pamoja na usemi. Wazungumzaji huwa na maoni tofauti kuhusiana na jambo fulani na huweza kuliangalia jambo hilo hilo kwa njia tofauti. Katika sarufi na semantiki, namna inahusu mbinu za kisarufi zinazoonesha kwa kiwango kipi jambo linalotazamwa ni la hakika, huenda likawa, labda, linawezekana, linaruhusiwa au linakatazwa. Usemi katika lugha, kwa kawaida, huelezewa kupitia vitenzi visaidizi vya hali. Endley (2010) anaeleza kuwa namna hutoa mtazamo wa mzungumzaji kuhusu tukio linaloelezewa.

### **Mtazamo wa kinadharia**

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Sarufi Amilifu Msonge (SAM) iliyoasisiwa na kuendelezwa na Halliday (1976, 1994, 2004) na inayojihusisha zaidi na wazo la uamilifu wa lugha. Ni nadharia inayojihusisha na maana kama uteuzi wa namna lugha au mfumo wowote wa kisemiotiki unavyoelezewa kama mfumo uunganishao uchaguzi – kama njia ya kuleta maana. Nadharia hii hujihusisha na muundo wa kisintaksia. Huangalia uamilifu wa lugha kama ulio muhimu sana (kile lugha inafanya, na namna inavyofanya) kwa kuzingatia mielekeo ya kimuundo ambayo huziweka elementi za lugha na michanganyiko yake kama yenye umuhimu mkubwa. Nadharia huanza kwa muktadha wa kijamii, na huangalia jinsi ambavyo lugha huyashughulikia majukumu yake, jambo ambalo hulazimishwa na muktadha wa kijamii. Kishazi huwasilisha matukio na mifanyiko ya namna mbalimbali na uelekezi hudhamiria kuweka wazi jinsi tendo linavyofanyika na anayefanya na kwa nani. Uelekezi ni dhana muhimu ya Halliday ya kisemantiki. Ni sehemu ya jukumu la kidhana la lugha na hivyo kigezo muhimu katika uchanganuzi wa uwasilishaji. La muhimu ni kuwa miundo muhimu ya kijamii huhitaji aina mbalimbali za uelekezi.

Jukumu la kimahusiano linaendana na jukumu la kimawasiliano linaloanzishwa na mzungumzaji likilinganishwa na la wengine. Jukumu linaweza kuelezwa kama njia ya uunganishaji wa mahusiano ya kijamii na maana kupitia lugha (au ‘tendo la usemaji’). Jukumu la kimatini la lugha humaanisha kuwa usemi (kama jukumu la kwanza na la pili la lugha) huwezekana kwa sababu wazungumzaji wanaweza kutoa matini kwa kuitumia na msikilizaji au msomaji anaweza kuitambua matini hiyo. Kulingana na Fowler (1991), lugha hufanya miungano kupitia lugha yenyewe na tukio lililopo au muktadha husika. Mawazo ya nadharia ya Sarufi Amilifu Msonge yalituongoza kuchunguza uwezekano wa ubishi wakati wa mawasiliano kati ya walezi na walelewa kwenye nyumba za watawa za malezi.

Hili linafanywa kwa lengo la kuangalia majukumu ya lugha yanayotekelezwa kupitia matumizi ya lugha kwenye nyumba za malezi ambapo kuna mahusiano ya kijamii yenye mamlaka yanayohitaji kuiunganisha jamii kupitia lugha. Hivyo, nadharia hii ndiyo ilitumika katika kutafiti suala la ubishi kwenye mahusiano ya kimamlaka katika nyumba za malezi. Utafiti

huu ulivitumia vipengele vya kisarufi kuchunguza dhamira na namna katika kuangalia namna lugha inavyotumiwa katika nyumba za malezi kudhihirisha mahusiano ya kimamlaka yanayotarajiwa kuwa yamefichwa kulingana na Fairclough (1989, 2000, 2010) kati ya walezi na walelewa na mahusiano haya ya kimamlaka yakadhihirisha ubishi. Ubishi huu unaweza kudhihirishwa kupitia matumizi ya lugha ya walezi na walelewa na kuonekana kama jambo la kawaida kupitia namna lugha inavyotumika. Sehemu ifuatayo inaangazia dhamira na namna inavyowasilisha mahusiano na mamlaka yaliyo na ubishi katika nyumba za watawa za malezi.

### **Dhamira na namna katika udhihirikaji wa mamlaka na mahusiano yaliyo na ubishi**

Majukumu ya kiuamilifu yanahusu matumizi ya lugha katika kuelezea mahusiano ya kijamii na ya kibinafsi (Halliday, 1985). Halliday anaeleza kuwa mzungumzaji hutumia lugha kama njia ya kuingiza katika tukio la mazungumzo: uelezaji wa maoni, mitazamo na tathmini na uhusiano anaouweka kati yake na msikilizaji; na kwa njia ya pekee nafasi ya mawasiliano ambayo anayakusudia kuyafahamisha, kuuliza maswali, kusihi na mengineyo. Utafiti huu ulielekezwa na madai haya na unayatumia kuchunguza jinsi ubishi na mahusiano ya jamii yanavyoweza kuelezewa kupitia dhamira na namna. Matei (2008) anaeleza dhamira kama kipengele cha kisarufi na kimaana ambacho huonesha lengo au maana inayoibuliwa na vitenzi mbalimbali katika sentensi. Fillmore (1968) anaeleza kuwa dhamira inaweza kuelezewa kama inayoundwa na kategoria mbili ambazo ni vitenzi vya hali pamoja na dhamira arifu, ulizi na agizi.

### **Dhamira ulizi**

Kama ilivyotajwa awali, mlezi katika kutumia dhamira ulizi anachukua jukumu la yule anayeuliza maswali na anamweka msikilizaji wake ambaye ni mlelewa katika nafasi ya yule anayetakiwa kujibu maswali. Jambo hili linamfanya mlezi kuonekana kama mwenye mamlaka kuliko mlelewa. Mlezi anadhihirika kama mwenye kuhitaji majibu ya "ndiyo" au "la" kutoka kwa walelewa jambo ambalo haliwezi kufanyika kinyume chake. Mlelewa, kwa upande mwingine, hawezi kutarajia jibu la "ndiyo" au "la" kutoka kwa mlezi. Mukstadha huu wa

mazungumzo unakuza mahusiano ya kijamii yanayodhihirisha mamlaka. Hili linadhihirika katika mfano ufuatao:

1. Uaminifu katika maisha yetu ni wa muhimu; neno letu liwe “ndio”; “ndio” kutoka moyoni na “la”; “la” kutoka moyoni. Mnasikia? Ndio sista. Kama unamaanisha “ndio” na iwe “ndio” na kama ni “la” iwe “la” kwa sababu itakuwa vibaya sana utakaposema “la” na kumbe unamaanisha “ndio”, utakuwa unadanganya nani? Mimi mwenyewe? Hapana sista. Unajidanganya? La. Ukijidanganya si wewe mwenyewe utabaki na kilio cha roho ndani ya moyo wako? Ndio sista.

Kauli hii ambayo ni maneno kutoka kwa mlezi wa makandidati wakati wa mafunzo kwa walelewa inaonesha kuwapo kwa mamlaka. Maswali yake yanamweka mlelewa katika hali ya kutakiwa kujibu swali kuhusu kinachozungumziwa ambacho ni kuwa mwaminifu maishani kwa kusema wazi anachokisema. Mzungumzaji ambaye ni mlezi anatumia dhamira ulizi na hivyo kumtoa mwenye mamlaka. Kupitia kauli yake, hata hivyo, kunadhihirika ubishi kwa kuwa matarajio yake kwa walelewa ni uaminifu ilhali walelewa hawa wako katika hatua ya kwanza ya maisha na bado hawajafaulu kuwa wanachama au bado hawajaelewa maisha jinsi yalivyo. Mlezi huyu, aidha, ametumia dhamira arifu katika kuwaelezea kuhusu uaminifu wanaopaswa kuwa nao katika maisha na walisemalo liwe ‘la’ kama ni ‘la’ na ‘ndiyo’ iwapo ni ‘ndiyo’.

Uchunguzi wa dhamira, kwa hivyo, siyo muhimu tu kwa kutafuta ni mawazo gani yanayotiliwa mkazo au yasiyotiliwa mkazo kwenye usemi fulani lakini katika kudhihirisha jinsi watu wanavyojitambulisha na kujipatia nafasi katika usemi husika kama inavyotokea kupitia kwa maneno ya mlezi. Uchunguzi wa namna unaonesha umuhimu wake wakati wa mahusiano ya kimamlaka kwa kuwa kupitia namna, mtu anaweza kwa mfano, kujua ni dhana zipi zinazotiliwa mkazo au kutotiliwa mkazo kuhusu mamlaka.

### **Namna katika kishazi**

Kulingana na Halliday (1985), matini ya kisarufi ambayo hutumiwa kama msingi wa uchanganuzi katika Sarufi Amilifu Msonge ni kishazi. Kishazi kimetambuliwa kuwa kipashio kidogo kwa mujibu wa Crystal (1985) na Radford (1997) katika sarufi ambacho kinaweza kuchanganuliwa katika muktadha wa mawasiliano. Hivyo, namna inaweza kujidhihirisha kwa aina mbalimbali kwenye kishazi; kwa mfano, kupitia vitenzi, kivumishi na aina fulani za

unominishaji. Fowler (1985) anatoa orodha ya kuelezea juu ya kategoria hizi. Kwake, namna inajitokeza kwa kishazi kupitia idadi ya miundo ya kisarufi, kama vile;

a. Vitenzi visaidizi vya hali, kama vile, nitakwenda, huna budi kwenda na kadhalika vinaonesha wakati ujao au ulazima. Hii inadhihirika katika mfano ufuatao:

2. Tunasema maisha tumeanza leo na tunaendelea mbele hakuna kurudi nyuma, kila siku jiambie, *nitakwenda* mbele, eee mtu akichukua jembe kwenda kulima anaangalia nyuma? Hapana, si anaendelea? Ndio, ukiangalia nyuma utaweza? Hapana, utaanza kuogopa. Kwa hivyo, tumwangelie Kristu yule aliyetuita.

Mfano (2) ambao ni kauli ya mlezi wa Mapostulanti wakati wa mafunzo unadhihirisha kitenzi cha hali *nitakwenda*. Kitenzi hiki kinaonesha ulazima anaotakiwa kufanya mlelewa ili kufaulu na hivyo kumpa mamlaka ya kuyatawala maisha yake ikiwa pia ni njia ya ubishi kwani katika maisha ya utawa anafaa kuelekezwa na mlezi. Kauli hii, aidha, inaonesha wakati ujao wa kitenzi kama njia ya matarajio ya kufaulu.

b. Sentensi elezi kama vile, huenda, yakini, kujutia na kadhalika. Hii inadhihirika katika mfano ufuatao:

3. Kwa hivyo, kila tendo unalolifanya, sadaka ndogo ndogo ni sifa na utukufu kwa Mwenyezi Mungu, si ya wanadamu, ni sifa na utukufu kwa Mwenyezi Mungu. Unapopangusa sahani hapa unapangusa kwa upendo, *huenda* kupangusa sahani eee, kupangusa tu, kukakupeleka mbinguni, unapangusa meza unapangusa kwa upendo, unahudumia mwenzako hata utampatia mwenzako glasi ya maji kwa upendo, hapo unahubiri Injili, unahudumia Kristo.

Mfano (3) ambao ni kauli ya mlezi wa Mapostulanti wakati wa mafunzo umetumia kitenzi cha hali *huenda* kinachoonessa hali ya uwezekano na kutoa dhamira ya namna ambayo inampa mlelewa matumaini ya kitendo anachokifanya kumpeleka mbinguni. Kitenzi hiki, aidha, kinampa mlelewa mamlaka ya kujitafutia maisha ya mbinguni ambayo mlezi hawezi kumpa ila kupitia jitihada zake mwenyewe.

c. Kirai nomino na kirai husishi kama vile lazima, bahati mbaya, bila shaka na kadhalika. Hii inadhihirika katika mfano ufuatao:

4. *Lazima* wewe mwenyewe ujikubali vile ulivyo; angalia unyonge wako, angalia furaha zako au vile vipaji vyako umepewa na Mwenyezi Mungu ndiposa Mungu amekuita katika shirika letu vipaji hivyo uweze kushirikisha jumuiya uweze kuvitoa kwa ajili ya wengine, vipaji tumepewa si vyetu wenyewe ni vya Mungu na ametupa kwa ajili tuweze kusaidiana hasa tunapoishi katika jumuiya.

Kauli hii, katika mfano wa (4), inatoka kwa mlezi wa Makandidati wakati wa mafunzo. Kirai nomino *lazima* kinaonesha wajibu ambao mlelewa ambaye ni mpokeaji wa tendo ana lazima ya kutimiza. Mlezi anadhihirisha mamlaka kwa kuonesha ulazima huu. Wajibu wa mlelewa ni kujikubali jinsi alivyo ambapo asipofanya hivyo hataweza kutumia vipaji vyake vizuri kwa ajili ya jumuiya. Hali hii ya wajibu wa mlelewa inamweka katika hali ya kuwa na mamlaka ya kufanya uamuzi kuhusu hali ya maisha yake na hivyo kudhihirisha ubishi.

d. Vitenzi vingine na unominishaji kama vile ruhusu, bashiri, thibitisha, wajibu, uwezekano, uteuzi, uongozi na kadhalika. Hili linadhihirika katika mfano ufuatao:

5. Asante kwa kushirikisha. Somo hili linatusukuma tutafakari maisha ya jumuiya. Tumeitwa tependane, *uteuzi* huu si wa mtu mwenyewe ila Yesu aliyetuchagua, tuishi kwa amani na ndani ya Kristo, na Kristo ndani yetu na tufanye *wajibu* wetu kwa upendo, yote kwa ajili yake. Tutafurahia wanangu nawaambia eeh sisi tunajua raha hiyo.

Mfano wa (5) ni kutokana na kauli ya mlezi wa Makandidati ambayo inadhihirisha matumizi ya nomino *uteuzi* na *wajibu*. Kupitia mfano huu, kauli ya mlezi inadhihirisha ubishi kwa kuwa anatomia hali ya ujumlishaji wake pamoja na walelewa na wote wanajiweka sawa katika kuonesha maana inayojitokeza kupitia nomino hizo. Kwamba, wote wana *wajibu* wa kupenda ili kuufurahia *uteuzi* wao. Hata hivyo, kwa mtazamo wa uchanganuzi hakiki usemi, maelezo ya dhamira yanahusu zaidi ya vitenzi visaidizi vya hali. Hili ni kwa sababu namna inatumiwa kutoa mitazamo na hali ya kujiamini kwa mzungumzaji kuhusu kauli yake kama ilivyodhihirika kwenye mfano huu wa mlezi wa Makandidati. Namna hugawanywa katika makundi mawili ambayo ni namna ya wajibu au shina inayohusu wajibu alionao mtu na namna ya kiufahamu inayohusu uwezekano.

## Namna ya Wajibu

Kulingana na Kreidler (1998), *namna ya wajibu* ni aina ya namna yenye umuhimu wa mtu kufanya au kutofanya kitu kwa njia fulani. Inadhihirisha iwapo kauli inayotolewa kupitia amri ni ya lazima, kushauriwa au ya kuruhusiwa kulingana na baadhi ya ufahamu wa kidehuri wa awali kama vile sheria, maadili, ukawaida na kadhalika. Aina hii ya namna inaelezea uamuzi wa mzungumzaji kulingana na wajibu (kimaadili au kijamii), ruhusa au makatazo. Vitenzi vyake hubeba maana inayohusiana na uwezo wa kuongoza mambo. Aina hii ya namna inaelekezwa kwenye dhana fulani ya wajibu, ruhusa, matamano, uwezo na kadhalika kama inavyodhihirika katika nyumba za malezi za watawa. Hili linadhihirika katika mfano ufuatao:

6. Mungu amekuita *lazima* utii haya mambo vizuri, kwa hivyo, tunataka kusaidiana tuishi maisha yetu, sawa? Ndio, na kila mtu *lazima* afurahie maisha na mimi nitakapokuwa hapa nanyi nione hamna raha basi itaniambia kuna kitu ambacho si sawa. Mfano (6) ambao unatokana na kauli ya mlezi wa Makandidati, *lazima* ni kitenzi cha hali cha namna kinachoelezea namna ya wajibu; kuwa wajibu wa kimaadili au kijamii *lazima* utimizwe na mpokeaji (Langacker, 1991). *Wajibu* hapa ni wa mbele kutii anayoambiwa pamoja na kufurahia maisha aliyoyachagua. Kupitia kauli hii mlezi anaoneshwa kama aliye na mamlaka ya kuelezea walelewa wanalopaswa kufanya kwa *lazima* isipokuwa mamlaka haya yanadhihirika kwa wote anaposema kuwa ‘*tunataka tusaidiane tuishi maisha yetu*’. Jambo hili linawaweka wote sawa mlezi na walelewa na kuwafanya wote kuwa na kiwango fulani cha mamlaka hivyo kuudhihirisha ubishi. Hii inaweza kuwa nafasi ya upingaji usio wazi wa mahusiano ya kimamlaka.

Vitenzi vya hali vya Kiswahili vinakubaliana na hali ya mtu binafsi kwa kile kinachohusika katika utendaji au kiima katika vitenzi kama vile *ninaweza*, *unaweza* na *anaweza* ambapo kinachooneshwa kinachotenda au kiima ni *ni-* katika *ninaweza*, *u-* katika *unaweza*, na *a-* katika *anaweza*. Namna hii ya wajibu inaonesha hamu ya mzungumzaji kwenye kauli anayoitoa kupitia uzungumzaji kama inavyodhihirika kwenye mifano ifuatayo:

7. Sasa tunataka ...ina hatua tano...Wacha tuone. Maana tunapoanza sala yetu ya moyo asubuhi tunafuata hatua hizi kwa mpangilio ili kufaulu katika sala ya moyo na sala ya moyo kamilifu...Kuna hatua tano. Wewe, *unaweza* kusoma ukurasa wa 33 kuhusu hatua?



Kauli hii ya mlezi wa Manovisi wakati wa mafunzo katika mfano (7) inayomwonesha mzungumzaji kama mwenye hamu ya kupitisha ujumbe kwa walelewa na pia kuwaruhusu kusoma anaposema *unaweza*. Hii pia ni njia ya kumpa mamlaka ya ujuzi ambapo mlelewa hawezi kumwambia mlezi kuwa *unaweza*. Hapa, mtendaji wa tendo la kusoma ni mlelewa anayewakilishwa na kiambishi *u-* katika kitenzi *unaweza*. Utendaji huu unampa mamlaka ya kutenda tendo la kusoma japokuwa ni mamlaka yasiyo wazi kwa kuwa anayetazamiwa kuwa msomaji ni mlezi mwenye ujuzi wa kitaasisi hivyo kuudhihirisha ubishi kwa kuwa mlelewa pia ana mamlaka ya usomaji. Jambo hili, aidha, linaonesha kuwa litatendeka wakati ujao.

8. Nani *anaweza* kukumbuka tulivyoambiwa na sista?

Vipindi vyote *vinapaswa* kutekelezwa kama ilivyo kwenye ratiba.

Katika mfano wa (8) inaonesha mtazamo wa mzungumzaji ambaye ni mlelewa na ambaye ni kiongozi wa mwezi kuwa ni muhimu vipindi vyote vifuatwe kulingana na ratiba. Anadhihirika mwenye mamlaka kupitia dhamira ulizi na kutarajia jibu kutoka kwa wenzake. Kitenzi *anaweza* kinamtoa mwenzake kama mtendaji. Inadhihirisha kauli inayotolewa na mlelewa kama yenye kuwashauri jinsi wanavyopaswa kufuata vipindi kwenye ratiba. Kauli zake zinatoa ubishi kwani anaonekana kama aliye na mamlaka dhidi ya wenzake.

Kulingana na Saeed (2003:136), namna ya wajibu inaweza kuwasilisha aina mbili za ujuzi wa kijamii ambazo ni wajibu na ruhusa. *Wajibu* unahusika na ‘kile mtu lazima atende’ ilhali *ruhusa* inahusiana na ‘mamlaka ya mwingine ya kuruhusu mtu mwingine kutenda jambo’. Nomino *lazima, sharti*, na vitenzi *yanipasa, nahitaji* na *itanipasa* katika mifano (9), (10) na (11) yote ni wajibu ilhali *unaweza, ungeweza, ungepata* ni ruhusa katika mifano (12) na (13).

Kila mwezi katika nyumba za malezi za shirika la Masista la Mtakatifu Yosefu kulingana na taratibu zilizowekwa huwa kuna mlelewa mmoja anayewaongoza wenzake. Na hili hufanywa kwa zamu kama njia ya kuwaandaa katika majukumu mbalimbali baadaye. Ikilinganishwa na mazungumzo ya walezi, walelewa wanaopewa majukumu ya kuongoza kwa mwezi wanaongea machache sana ikilinganishwa na walezi kama njia ya kudhihirisha ubishi. Walelewa, baada ya kikao cha mazungumzo, wanaombwa na mlezi wazungumze na wanajitolea kusema jambo.

Wanaongea kwa kifupi sana kumshukuru mlezi aliyewashauri katika mazungumzo. Jambo hili linatendeka wakati mlezi na walelewa wako pamoja.

9. Kiongozi wa mwezi: Sista na Makandidati tumsifu Yesu Kristo?  
Wote: Milele Amina.  
Kiongozi wa mwezi: Kwa niaba ya walelewa nataka kushukuru sista kwa yale yote aliyotuambia. Tunaahidi kushika yote uliyotuambia. Tufanye bidii. Binafsi *nahitaji* kujitahidi pia.  
Kiongozi wa mwezi: Mnakubaliana nami?  
Wote: Ndio.  
Kiongozi wa mwezi: Asanteni sana.

Katika mfano (9) ambao ni kauli ya mlelewa ambaye ni mkubwa wa mwezi, matumizi ya kitenzi cha hali *nahitaji* yanaonesha wajibu alionao katika kufanya jitihada kutekeleza waliloambiwa na mlezi. Licha ya kuwa anawashauri wenzake, yeye pia ana wajibu wa kutekeleza anayowaambia. Maneno ya kiongozi wa mwezi yanatoa mamlaka aliyonayo dhidi ya wenzake kwa kuwa yeye ndiye anayetegemewa katika kushauri na kuongoza wenzake kwa kipindi cha mwezi mmoja. Hali hii inadhihirisha ubishi kwa kuwa mwenyewe anatazamiwa kuelekezwa na mlezi ilhali naye analo jukumu sawia la kuwaelekeza wenzake. Iwapo kuna lolote litakaloenda kinyume, yeye ndiye anayewajibika na kuulizwa na mlezi. Mlelewa huyu anakaa kuwa juu ya wenzake kingazi hivyo mwenye mamlaka dhidi ya wenzake. Hili linadhihirika katika matumizi yake ya lugha kwa kuwa anaongea kwa niaba ya wenzake anaposema, *kwa niaba ya walelewa nataka kumshukuru sista kwa yale yote aliyotuambia. Tunaahidi kushika yote uliyotuambia. Anatumia dhamira arifu kuelezea alichonacho. Jambo hili linajitokeza pia katika mfano (10) anapotumia kitenzi cha hali tunapaswa* kinachodhihirisha wajibu walionao katika kuchukuliana sawa.

10. *Tunapaswa* kuchukuliana sisi sote sawa, si ati kwa sababu wewe ni mtaita unataka kukaribia sista mlezi na unajua kuna tatizo lingine; kuna watu ambao wakikaa katika kikundi kama hiki wanataka kupendwa... si mwawajua? *Yanipasa* nijue sitegemei mlezi. Maisha ni mimi mwenyewe. *Itanipasa* nifanye uamuzi mwenyewe ili kufaulu bila kuegemea wengine au mlezi.

Katika mfano (10) ambao ni kauli kutoka kwa mlezi inadhihirisha wajibu wake pamoja na walelewa katika kuyaishi maisha wanavyopaswa. Anatumia vitenzi vya hali *tunapaswa*,

*yanipasa* na *itanipasa* kama udhihirishaji wa wajibu. Licha ya kuwa anawaongoza walelewa anajitia ndani ya anachokisema hivyo kudhihirisha ubishi wa kuwaweka sawa kimamlaka na hivyo kutoa mamlaka yaliyofichwa.

11. Mara moja baada ya misa ya jioni ni kimya kuu, *sharti* uwe kimya kwa sababu ya tafakari ya asubuhi ili uwe umejikusanya kwa sababu huwezi kuanza kwenda kupiga hadithi leo hivi unasumbuliwa, si ndio? ...unasumbuliwa hiyo ili uwe umejikusanya *lazima* uzingatie kimya...*lazima* uzingatie kimya...sio mzaha hapa!

Mfano (11) wa kauli ya mlezi wa Manovisi wakati wa mafunzo unaonesha kile mlelewa lazima atende kupitia matumizi ya vitenzi vya hali vya *lazima* na *sharti*. Anachopaswa kukitenda ni kudumisha kimya kuu ambao ni wajibu na unamtoa mzungumzaji ambaye ni mlezi wa Manovisi kama mwenye mamlaka kupitia matumizi ya dhamira agizi na ulizi.

12. Kutoka sasa tunza wito wako, sawa? Ndio. *Ungepata* nafasi saa hii *ungeweza* kuondoka? Najua la kabisa! Endelea basi na wito wako. Sawa?

13. Ni wewe ulichagua kifungu hicho kwa hiyo sala (anaingilia kati), uache maneno yaingie ndani. *Unaweza* kurudia, hauhitaji kuwa na kifungu kirefu...la kifupi tu halafu urudie tena.

Katika mfano (12) ambayo ni kauli ya mlezi wa Makandidati wakati wa vikao vya kuwaelekeza, matumizi ya vitenzi *ungepata* na *ungeweza* vinawasilisha ujuzi wa kijamii wa *ruhusa* unaohusiana na mamlaka ya mlezi ya kuruhusu mlelewa kutenda jambo. Hili pia linajitokeza katika mfano (13) wa mlezi wa Manovisi kupitia matumizi ya kitenzi *unaweza* kama njia ya kutoa ruhusa.

### **Namna ya kiutambuzi**

Kreidler (1998) anaeleza kuwa namna ya kiutambuzi inahusu uwezekano, hali ya kuwa au kutowezekana kwa kauli fulani. Ni namna inayohusu utathmini na hukumu ya mzungumzaji kuhusiana na kiwango cha kujiamini cha ujuzi wa kauli. Inafanya kazi kuelezea au kutathmini ufafanuzi wa uhalisia katika utekelezaji wa majukumu ya uzungumzaji. Ni aina ya utambulishi wa kisarufi unaoonesha uamuzi wa mzungumzaji unaotokana na ujuzi wake wa uwezekano,

uelekeo au uhakika wa kauli inayoelezewa katika sentensi kama asemavyo Langacker (1991). Kwa mfano, katika Kiswahili, vitenzi vya hali vya kiutambuzi ni kama vile *atakuwa*, *anaweza*, *huenda* na kadhalika. Hili linadhihirika katika mfano ufuatao:

14. Unapopangusa sahani hapa unapangusa kwa upendo, ***huenda*** kupangusa sahani eee, kupangusa tu, kukakupeleka mbinguni, unapangusa meza unapangusa kwa upendo, unahudumia mwenzako hata utampatia mwenzako glasi ya maji kwa upendo, hapo unahubiri Injili, unahudumia Kristo.

Kitenzi cha hali cha kiutambuzi *huenda* katika mfano (14) kinaonesha kuwa mzungumzaji ambaye ni mlezi anaelezea msikilizaji wake ambaye ni mlelewa uwezekano kuwa wazo au fikra zinazoelezewa kwake zinaweza kusaidia au kuwa muhimu wakati wa baadaye kama vile kufanya kitendo cha kupangusa sahani. Kitenzi hiki cha hali cha kiutambuzi kinatambuliwa wakati jukumu lake kuu ni kudhihirisha uwezekano wa namna inayokusudiwa kuonesha kuwa kuna uwezekano kuwa wazo linaweza kuwa la kufaa na lenye maana siku za baadaye na siyo wakati huu. Walelewa katika kumfuata Kristo na kuwa watawa wana lengo la hatimaye kwenda mbinguni. Hivyo, kauli hii ya mlezi wa Mapostulanti inatoa uwezekano wa wazo analowaelezea walelewa la kupangusa sahani likawasaidia kufika mbinguni na hili litawezekana baadaye. Kauli hii ya mlezi inaonesha ubishi wa kutokuwa na uhakika wa kile kitatokea baadaye licha yeye kuwa na mamlaka ya kiujuzi na kitaasisi.

15. Hayo mambo hatutaki, nataka utangamano wa hali ya juu kwamba kila mtu *anaweza* kutangamana na yule mwingine, haya maisha hakuna mtu atakwambia chagua hiki, chagua huyu, ufanye hivi, uamuzi ni wako peke yako.

Katika mfano (15) ambayo ni kauli ya mlezi wa Makandidati wakati wa vikao vya kuwaelekeza walelewa, matumizi ya kitenzi cha hali *anaweza* kinawasilisha uwezekano wa kila mtu kutangamana na mwingine. Wazo hili la utangamano linaweza kuwa la kufaa na lenye maana siku za baadaye miongoni mwa walelewa.

16. Mlelewa Msimamizi mkuu wa sherehe (Mpostulanti): Mtoto wetu wa siku moja *anaweza* kukata keki...

Mfano (16) unatokana na kauli ya mlelewa anayeelekeza shughuli wakati wa sikukuu ya kumbukumbu ya sikukuu ya kuzaliwa kwa mlezi wao. Hiki ni kikao cha hali ya kawaida katika maisha haya ya malezi. Katika burudisho kwenye wimbo wao *‘Tumetoka sehemu mbalimbali’* wakati wa sikukuu ya kuzaliwa kwa mlezi wa Mapostulanti, walelewa wanamwendea mlezi ambaye anasherehekea sikukuu yake na wanamwita *mtoto wa siku moja* bila kuonesha kujali kama ni mlezi kwa kuwa kipindi hiki ni cha sherehe. Hali hii inadhihirisha ubishi kwa kuwa katika kawaida ya maisha ya utawa hawawezi kumwita mlezi mtoto na iwapo watafanya hivyo wataonekana kama wenye dharau. Inadhihirika pia hawasemi mengi kuhusiana na hali hiyo ya kumwita mlezi mtoto wasije wakaenda kinyume cha wanavyopaswa kutenda. Matumizi ya kitenzi cha hali *anaweza* kinawasilisha uwezekano wa mlezi anayerejelewa kama mtoto wa siku moja kuweza kukata keki. Wazo hili la kukata keki linaweza kuwa la kufaa na lenye maana baadaye.

17. Tunaendelea tulipoachia, unakumbuka si kitambo kabla ya kwenda chai? Huwezi *kuwa* umesahau hakika, nani anakumbuka? Nani?

Mfano (17) unatoa kauli ya mlezi wa Manovisi wakati wa mafunzo na unaonesha hali ya kutowezekana au ya kutokuwa. Jambo ambalo walelewa haiwezekani kuwa wawe wamesahau kile walichokuwa wanafunzwa muda uliopita kabla ya kwenda kunywa chai. Kulingana na Saeed (2003) tofauti kati ya namna ya wajibu na kiutambuzi hata hivyo mara nyingine haioneshi tofauti kwa kuwa zote zinaweza kudhihirishwa na vitenzi hali vilivyo sawa kama inavyodhihirika kwenye mfano ufuatao:

18. *Unaweza kusoma Biblia hiyo.*

Maana ya mfano (18) unaweza kuwa: Una ruhusa yangu ya kusoma Biblia hiyo au kuna uwezekano unaweza kusoma Biblia hiyo. Hali hii inaonesha maana ya kwanza inayodhihirisha namna ya wajibu ilhali ya pili ikionesha namna ya kiutambuzi.

### **Ukanusho wa namna**

Kreidler (1998) anaeleza kuwa ukanusho unaweza kuchanganyika na namna. Utokeaji wa *si* na kitenzi cha hali unaweza kukanusha kitenzi hali chenye au ujumbe wa kauli inayofuata.

Mifano (19) na (20) inaonesha ukanusho katika namna ya wajibu ilhali (21) na (22) unaonesha ukanusho katika namna ya kiutambuzi.

19. Uimbaji mzuri utajisikiliza wewe mwenyewe ili sauti yako *isiende* juu ya wengine au *isiende* chini ya wengine, *usipaze* sauti ila iwe kadri au wewe ni mwimbaji mbaya?

20. Kama umeamua kuja, kuja kabisa na huwa naambia watu ukiamua kuogelea *si* lazima uogeleee? Ndio, wee ushaona mtu anaenda kuogelea na anaingia na lesa? Hapana, *si* lazima aingie kuogelea vizuri? Ndio, nyinyi si mmeamua kuogelea katika shirika hili?

Katika mfano (19) kauli inadhihirisha kuwa “*kutopaza* sauti ni wajibu wako”. Kwa maneno mengine, vitenzi vya hali *usipaze* sauti na *isiende* vinaonesha kukatazwa, hivyo ukanusho unajitokeza katika kauli. Katika mfano wa (20), inaonesha ukanusho unaodhihirisha kuwa “siyo lazima kuogelea” na hivyo, mzungumzaji anampa msikilizaji uamuzi kuwa “unaweza kuogelea lakini si lazima”.

21. Ninawaambia kesho tutapata Mama Mkuu kutoka hapa, sawa? Mama Mkuu *si* lazima awe huyu unayefikiria kwa kichwa chako.

22. La, Mama Mkuu *hawezi* kuwa kwa hewa tu...

Katika mfano (21) kauli inaonesha uwezekano wa Mama Mkuu kutokuwa kwa kichwa cha mlelewa anayemfikiria ilhali (22) inaonesha ugumu wa Mama Mkuu kuwa hewani. *Si* katika (21) inaonesha hali iliyoko kwenye kauli ilhali (22) *si* inadhihirishwa kwenye kitenzi cha hali *hawezi*.

## **Hitimisho**

Utafiti huu umebainisha kuwapo kwa mahusiano ya kimamlaka yenye ubishi katika nyumba za watawa za malezi kupitia matumizi ya lugha. Aidha, umedhihirisha kuwa ubishi na mahusiano ya jamii yanaweza kuelezewa kupitia dhamira na namna kupitia vitenzi vya hali. Majukumu ya kiuamilifu yanayohusu matumizi ya lugha katika kuelezea mahusiano ya jamii ya walezi na walelewa na ya mtu binafsi yamedhihirika. Dhamira agizi, dhamira ulizi na dhamira arifu zimetumika kama njia ya kuonesha kuwa walezi na walelewa wanadhihirisha kiwango fulani cha mamlaka.

Kupitia matumizi ya lugha namna imejidhihirisha kupitia aina mbalimbali katika kishazi na sentensi; kwa mfano, kupitia vitenzi, kirai nomino na aina fulani za unominishaji. Kupitia namna kumedhihirika kauli za walezi na walelewa za wajibu na uwezekano. Hali hii inawaweka katika viwango tofauti kimazungumzo na kitaasisi na hivyo kudhihirisha mamlaka yasiyo na usawa kwenye nyumba hizi za malezi. Jambo hili ni njia isiyo wazi ya kudhihirisha ubishi. Walezi wamejitokeza kama wanaotumia namna zaidi hivyo kuwatoa wenye mamlaka dhidi ya walelewa. Kauli zao, aidha, kupitia namna zinadhihirisha uhakika, jukumu na wajibu wa kile wanachokisema kwa walelewa na wanatumia lazima jambo ambalo ni nadra kwa walelewa.

### **Marejeleo**

- Endley, M. J. (2010). *Linguistic Perspectives on English Grammar: A Guide for EFL Teachers*. Information Age Publishing.
- Fairclough, N. (1989). *Language and Power*. Longman.
- \_\_\_\_\_ (1992). *Discourse and Social Change*. Blackwell.
- \_\_\_\_\_ (2000). *Language and Power* (Toleo la pili). Longman.
- \_\_\_\_\_ (2010). *Critical Discourse Analysis: The Critical Study Language*. (Toleo la pili). Longman.
- Fowler, R. (1985). Power. In T. A. van Dijk (ed.), *Handbook of Discourse Analysis, Vol. 4*. Academic Press, Inc. pp.61-82.
- Fowler, R. (1991). *Language in the News. Discourse and Ideology in the Press*. Routledge and Kegan Paul.
- Halliday, M.A.K. na Hassan, R. (1976). *Cohesion in English*. Longman.
- \_\_\_\_\_ (1985). *An Introduction to Functional Grammar*. Edward Arnold.
- \_\_\_\_\_ (1994). *An Introduction to Functional Grammar* (Toleo la pili). Edward Arnold.
- \_\_\_\_\_ (2004). *An Introduction to Functional Grammar* (Toleo la tatu). Edward Arnold.
- Kreidler. (1998). *Introducing English Semantic*. Routledge.
- Langacker, R.W. (1991). *Foundations of Cognitive Grammar Vol. II Descriptive Application*. Stanford University Press.

- Matei, A.K. (2008). *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi Kamili wa Sarufi ya Kiswahili*. Phoenix Publishers.
- Radford, A. (1997). *Syntactic Theory and the Structure of English*. Cambridge University Press.
- Saeed, J. L. (2003). *Semantics*. 2<sup>nd</sup> ed. Blackwell Publishing.
- Wodak, R. (2001). “*What CDA is about – A summary of its History, Important Concepts and its Developments*” katika Wodak, R. & Meyer, M. (Wah.). *Methods of Critical Discourse Analysis*. Sage Publications Ltd. 1-13.